**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

***Dodoma***
***18 Novemba, 2025***

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa kazi kubwa iliyopo mbele ya Mawaziri na Naibu Mawaziri ni kuwajibika kwa wananchi na Taifa kwa ujumla, akisisitiza kuwa dhamana waliyokabidhiwa sio nafasi ya fahari bali ni kazi ya utumishi kwa Watanzania.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo wakati akiwaapisha Mawaziri na Naibu Mawaziri Wateule katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Dkt. Samia amewashukuru na kupongeza kazi nzuri iliyofanywa na viongozi waliomaliza muda wao katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Sita na amewatakia heri viongozi wapya walioapa.

Halikadhalika, amewataka viongozi hao kuwa mfano wa utu na uadilifu katika utendaji wao na kuonya kuwa hatasita kuwawajibisha watakaoshindwa kutimiza majukumu waliyopewa.

Vilevile, Rais Dkt. Samia amewaagiza Mawaziri na Naibu Mawaziri hao kushirikiana na Makatibu Wakuu wa Wizara zao kuanza mara moja utekelezaji wa ahadi za siku 100 ili wananchi waone matokeo ndani ya muda huo mfupi.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia amesema kuwa katika kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali itapunguza utegemezi kwenye mikopo na itaongeza nguvu katika kutumia rasilimali za ndani kutekeleza miradi yake ili kuhakikisha kasi ya maendeleo haiathiriwi na mabadiliko ya upatikanaji wa fedha kutoka nje.

Aidha, amewataka viongozi walioapa kujituma na kufanya kazi kwa bidii ili kuleta matokeo yanayoonekana na yenye tija kwa wananchi na kuhakikisha kasi ya utekelezaji wa miradi ya Serikali inaendana na matarajio ya wananchi.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu